

The
Management
University
of Africa



Sponsored by the Kenya Institute of Management

UNDERGRADUATE UNIVERSITY EXAMINATIONS
SCHOOL OF MANAGEMENT AND LEADERSHIP
DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION ARTS

KIS 325: RIWAYA NA HADITHI FUPI YA KISWAHILI

DATE: 1ST APRIL 2026

DURATION: 2 HOURS

MAXIMUM MARKS: 70

MAAGIZO :

1. Andika nambari yako ya usajili kwenye kitabu cha majibu.
2. **USIANDIKE CHOCHOTE kwenye karatasi ya majibu.**
3. Karatasi hii ya maswali ina **MASWALI SITA (6).**
4. Swali la **KWANZA** ni la lazima .
5. Jibu maswali yoyote **MATATU.**
6. **SWALI LA KWANZA** lina alama 25 na hayo mengine yana alama 15.
7. **Andika majibu yako yote kwenye kitabu cha majibu ulichopewa. .**

SWALI LA KWANZA

(A) Kwa kutoa mifano, fafanua aina zifuatazo za riwaya ya Kiswahili.

i) Ya tawasifu.

(alama 4)

ii) Ya tashtiti

(alama

4)

iii) Pendwa

(alama

4)

(B) Huku ukitoa mifano mwafaka, pambanua uhusiano na Tofauti zilizopo baina ya riwaya na hadithi fupi.

(alama

13)

SWALI LA PILI

Huku ukitoa mifano kutoka riwaya uliyoisoma darasani, jadili vipengele vya kifani ambavyo hutumiwa katika kuchanganua riwaya ya Kiswahili.

(alama 15)

SWALI LA TATU

a) Jadili sifa kuu za hadithi fupi ya Kiswahili huku ukitoa mifano kutoka kwa Diwani ya Hadithi fupi uliyoisoma darasani.

(alama 5)

b) Eleza sifa-tabia **tano** za mhusika mkuu katika **MOJAWAPO** wa riwaya zifuatazo.

(alama

10)

i) *Kiu . (S.A Mohamed)*

ii) *Kichwa Maji - (E. Kezilahabi)*

SWALI LA NNE

Tathmini ufaafu wa anwani ya **MOJA** kati ya riwaya zifuatazo.

(alama 15)

a) *Kidagaa Kimemwozea (Ken Walibora)*

b) *Chozi la Kheri - (Assumpta Matei).*

SWALI LA TANO

Fafanua maudhui matano yanayojitokeza katika **MOJAWAPO** wa riwaya zifuatazao **(alama**

15)

a) Kisima cha Giningi - (S.A. Mohamed)

b) Nguu za Jadi - (Clara Momanyi).

SWALI LA SITA

Kwa kutolea mifano mahususi, onyesha ni vipi fani na maudhui huingiliana katika fasihi. **(alama**

15)